# Serikali: Kuna matumizi mabaya ya vibali vya kusafirisha mifugo

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imekiri kuwapo kwa matumizi mabaya ya vibali vya kusafirisha mifugo kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine.

Wizara hiyo ilitoa kauli hiyo bungeni jana katika swali la Mbunge wa Madaba (CCM), Joseph Mhagama.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali itachukua hatua gani kudhibiti watu wanaodanganya kupeleka ng'ombe katika mnada wa Mtyangimbole kisha kuwatorosha na kuwaingiza katika maeneo mbalimbali ya Madaba, Namtumbo na Songea ilhali Madaba haina uwezo wa kuhimili wingi wa mifugo.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema wafugaji wanakata vibali vya kusafirisha mifugo kwenda mnadani kwa ajili ya biashara na kinyume chake inahamishwa kuelekea maeneo mengine ya mikoa ukiwamo mkoa wa Ruvuma Halmashauri ya Madaba.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa kwa kipindi cha kuanzia Aprili 2020 hadi Aprili 2021 idadi ya mifugo iliyosajiliwa katika Halmashauri ya Madaba yenye vibali kuelekea mnada wa upili wa Mtyangimbole ni ng'ombe 8,925 wakati walioingia mnadani ni 5,753.

Ilisema kuna tofauti ya ng'ombe 3,172 wanaosadikika kuingia katika maeneo mbalimbali na kusababisha migogoro.

Hata hivyo, wizara ilisema kwa kushirikiana na Halmashauri ya Madaba itaimarisha ufuatiliaji wa vibali vya mifugo ili kuhakikisha mifugo iliyoandikiwa vibali kwenda mnada wa Mtyangimbole imefika. Vilevile, ilisema katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo katika maeneo ya wafugaji, serikali imetenga Sh.milioni 193.28 kwa ajili ya utatuzi wa migogoro na utengaji wa maeneo ya malisho.

Pia, alisema Sh. bilioni 1.586 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa au malambo na visima virefu, ambapo katika Mkoa wa Ruvuma Halmashauri ya Songea kisima kimoja kitachimbwa kwa lengo la kuwapatia mifugo maji.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, serikali inaendelea kuwahamasisha wadau wengine wakimamo wafugaji kujiunga kwenye vikundi na kushiriki kwenye ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji na uendelezaji wa malisho katika maeneo yaliyotengwa ili kuzuia uhamaji usio wa lazima unaosababisha migogoro.

Scanned with CamScanner

# Minister demands investigation after livestock deaths

By DAILY NEWS Reporter

LIVESTOCK and Fisheries Minister Mashimba Ndaki yesterday ordered the veterinary council to investigate and hold accountable veterinarians, who caused some livestock to die or get adverse effects after vaccination at Mlazo village, Dodoma region.

Minister Ndaki issued the directive when he toured the Mlazo Village and after had received a report on aftermath of the cattle vaccination against Contagious Bovine Pleuropneumonia (CBPP).

"The vaccination led to the death of over 25 cattle, 33 abortions, 58 got swellings on injected parts of skin," he noted

Mr Ndaki argued that the on-going countrywide vaccination exercise has good intention, wondering how such incident happened at Mlazo village.

"I am disappointed with how they executed it in Mlazo village. They did not follow the laid procedures and guidelines," he stated.

The minister also suspended the Agristeps Limited, a company that entered contract with Chamwino District Council to oversee the immunization exercise, and also referred it to the Veterinary Council of Tanzania for further investigation.

"Thorough investigation must be conducted against the veterinarians who administered vaccination and measures taken against them. This company should also pay the costs for the menace it has caused," he noted.

In addition, Mr Ndaki has called on all councils in the country to ensure that service providers who have entered contracts to provide vaccination against 13 major livestock diseases follow the issued guidelines.

In January 2020, the ministry issued guidelines for the provision of vaccines against livestock diseases in the country aimed at ensuring animal health and safety.

Following the deaths and effects of vaccination, Mr Ndaki saw the need of amendment of the Veterinary Act 2003 and the Animal Diseases Act of 2003 to introduce compensations to livestock keepers.

The Director of Veterinary Services in the ministry, Prof Hezron Nonga said preliminary investigations revealed the needles used were too long that supposed to be injected on thick skin not thin skin as they did.

Some pastoralists who spoke at the meeting said the immunization exercise was conducted in their village in July 19, 2021 was not participatory since there was no provision of awareness education before the exercise.

They also complained over lack of co-operation from village leaders, saying the leaders only focused on raising funds for the vaccination.



*MR Ndaki*

Scanned with CamScanner